

Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Leordger Tenga, akifafanua jambo wakati akitangaza kamati za maadili za shirikisho hilo jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Katibu Mkuu wa TFF, Angetile Osiah. (Picha na Francis Dande)

# Mfaransa kujenga Academy Arumeru

Na Ramadhan Siwayombe, Arumeru

KITUO kikubwa cha soka cha kulea vijana wadogo 'Soccer Academy' kinatarajiwa kuanzishwa na mdau wa michezo kutoka nchini Ufaransa, Damian Sellier, katika eneo la Liganga mji mdogo wa Usa River wilayani Arumeru, mkoani Arusha.

Akizungumza na Tanzania Daima mjini hapa jana, Sellier alisema amelazimika kuanzisha kituo hicho baada ya kuvutiwa na wananchi wa eneo hilo kupenda michezo hususan soka, lakini wakikosa uwezo wa kuwandaa vijana wao kuwa wachezaji bora.

"Nilifika hapa na kuamua kushirikiana na kituo cha Usa River Youth kuanzisha mashindano maalumu ya vijana chini ya miaka 15 na chini ya miaka 20, ambapo watu wengi wamejitokeza kuyaunga mkono na hivyo kunifanya nishawishike kuanzisha kituo hicho cha vijana," alisema Damian.

Alifafanua kuwa mara baada ya kumalizika kwa mashindano hayo Agosti na yanayoshirikisha timu 14, ataondoka kwenda Ufaransa kwa ajili ya kuweka mambo sawa tayari kuanzisha kituo hicho atakaporejea akiwa na vifaa kamili.

Naye mratibu wa Usar river Youth, Daudi Mkumba, akizungumzia mpango huo alisema wao kama kituo kilichosajiliwa, waliamua kushirikiana na mdau huyo kusimamia mashindano aliyoyaanzisha kwa kuwa anapenda michezo.

"Huyu bwana anapenda mpira; akawa anataka kuanzisha mashindano ya vijana kwa kuwa hajawa na taasisi yoyote iliyosajiliwa hapa nchini, akaamua kuja kutushirikisha sisi ili tusimamie michezo hii kupitia taasisi yetu na tunaendelea naye vizuri," alisema Mkumba.

Alifafanua kuwa tayari Mfaransa huyo ana taasisi yake aliyoanza kuisajili iitwayo Help Development Sports For Tanzania Children, ambayo ndiyo itakuwa inamiliki kituo hicho anachotaka kuanzisha, ambapo pia ana mpango wa kujenga uwanja wa kisasa.

# Deogratius Lyato, Mtiginjola 'out' TFF

Inatoka Uk 24

Tenga alisema mabadiliko hayo pia yamegusa kamati nyingine mbili, yaani Kamati ya Nidhamu na Kamati ya Uchaguzi ambayo sasa itaongozwa na Mwanasheria Mkuu wa zamani wa Zanzibar, Hamidu Mbwezeleni, Jaji Ihema ataongoza Kamati ya Rufaa za Maadili akisaidiwa na mwanasheria mwingine mwandamizi, Victoria Makani, huku Bi. Mguto, ambaye anakuwa mwanamke wa kwanza kuongoza vyombo vya maamuzi ataongoza Kamati ya Maadili akisaidiwa na makamu wake, Francis Kabwe, ambaye ni Msajili wa Mahakama Kuu.

Katika uteuzi huo, baadhi ya wajumbe wamehamishwa kutoka kamati moja hadi nyingine, ambao ni Murtaza Mangungu kutoka Kamati ya Rufaa za Uchaguzi kwenda Kamati ya Rufaa za Maadili, Kamanda Mohamed Mpinga na Prof. Madundo Mtambo wamehamishwa kutoka Kamati ya Rufaa za Uchaguzi kwenda Kamati ya Maadili.

Wajumbe wapya kwenye kamati hizo ni pamoja na kocha wa zamani wa Taifa Stars na Reli ya Morogoro, Dk. Mshindo Msolla na Kamanda mstaafu, Jamal Rwambow, wanaingia kwenye Kamati ya Nidhamu, mwanasheria maarufu Evod Mmanda Kamati ya Maadili, mwanasheria mwandamizi Mustapha Kambona Kamati ya Nidhamu, Mohamed Misanga Kamati ya Maadili na Kanali mstaafu Iddi Kipingu, ambaye anasifika kwa kuendesha soka ya vijana, anaingia kwenye Kamati ya Rufaa za Nidhamu.

Pia Mwanasheria Anne Marealle anakuwa mjumbe kwenye Kamati ya Rufaa za Uchaguzi, Yohane Masale, Allen Kasamala na Francis Kiwanga Kamati ya Rufaa za Uchaguzi na mkufunzi wa Fifa, Henry Tandau Kamati ya Rufaa za Maadili.

Kamati ya Utendaji pia imefanya mabadiliko kwenye Kamati ya Waamuzi, ambako mwenyekiti Said Nassoro na katibu Charles Ndagala wa Chama cha Waamuzi (FRAT), wanaingia kwenye kamati hiyo kushika nafasi ya Joan Minja na Riziki Majala.

Wajumbe wa Kamati ya Rufaa za Maadili ni Jaji Steven Ihema (mwenyekiti), Victoria Makani (m/mwenyekiti), Mohamed Misanga, Tandau na Murtaza Mangungu, huku Kamati ya Maadili ni Jesse Mguto (mwenyekiti), Francis Kabwe (m/mwenyekiti), ACP Mohamed Mpinga, Prof. Madundo Mtambo na Evod Mmanda wakati Kamati ya Rufaa za Nidhamu ni Prof. Mgongo Fimbo (mwenyekiti), Ong'wanuhama Kibuta (m/mwenyekiti), Kipingu, Dk. Msolla na ACP Rwambow.

Kamati ya Nidhamu ni Tibaigana (mwenyekiti), Mustafa Kambona (m/mwenyekiti), Azzan Zungu, Yussu Nzowa na Mohamed Msomali huku Kamati ya Rufaa za Uchaguzi ni Jaji Bernard Luanda (mwenyekiti), Francis Kiwanga (m/mwenyekiti), A. Steven Semu, Yohane Masalla na Allen Kasamala.

Kamati ya Uchaguzi yuko Hamidu Mbwezeleni (mwenyekiti), Moses Kaluwa (m/mwenyekiti), Mustafa Siani, Hassan Dyamwale na Kitwana Manara.

Kamati ya Waamuzi ni Kapteni mstaafu Stanley Lugenge, (mwenyekiti) Omar Kasinde (m/mwenyekiti), Said Nassoro, Charles Ndagala na Mohamed Nyama wakati Kamati ya maadaktari itakuwa chini ya Maleare Paul, (mwenyekiti), Anthony Ngombe (m/mwenyekiti), Mwanandi Mwankemwa na Mshama Joakimu.

Alisema kuwa katika kamati hizo ambazo zamani zilikuwa na watu saba, sasa zitakuwa na watano na kuongeza kuwa, uteuzi huo umeangalia na hali ambayo ilijitokeza katika uchaguzi uliotangazwa hapo awali, ambao ulionekana kuleta hali tofauti na ilivyozoeleka katika Shirikisho hilo.






WAKUDATA

Na Said Michael

